# Yoeli

1 Neno la Mwenyezi Mungu ambalo lilimjia Yoeli mwana wa Pethueli.

*Kuvamiwa wa nzige*

2 Sikilizeni hili, enyi wazee;
sikilizeni, ninyi nyote mnaoishi katika nchi.
Je, jambo kama hili lilishawahi kutokea
katika siku zenu au katika siku za babu zenu?
3 Waelezeni watoto wenu,
na watoto wenu wawaambie watoto wao,
na watoto wao kwa kizazi kitakachofuata.
4 Kilichosazwa na kundi la tunutu
nzige wakubwa wamekula,
kilichosazwa na nzige wakubwa
parare wamekula,
kilichosazwa na parare
madumadu wamekula.

5 Amkeni, enyi walevi, mlie!
Pigeni yowe enyi wanywaji wote wa mvinyo,
pigeni yowe kwa sababu ya mvinyo mpya,
kwa kuwa mmenyang'anywa
kutoka midomoni mwenu.
6 Taifa limevamia nchi yangu,
lenye nguvu tena lisilo na idadi;
lina meno ya simba,
magego ya simba jike.
7 Limeharibu mizabibu yangu
na kuangamiza mitini yangu.
Limebambua magome yake

na kuyatupilia mbali,
likayaacha matawi yake yakiwa meupe.

8 Omboleza kama bikira aliyevaa gunia
akimwomboleza mume wa ujana wake.
9 Sadaka za nafaka na sadaka za kinywaji
zimekatiliwa mbali kutoka nyumba ya Mwenyezi Mungu.
Makuhani wanaomboleza,
wale wanaohudumu mbele za Mwenyezi Mungu.
10 Mashamba yameharibiwa,
ardhi imekauka;
nafaka imeharibiwa,
mvinyo mpya umekauka,
mafuta yamekoma.

11 Kateni tamaa, enyi wakulima,
lieni, enyi mlimao mizabibu;
huzunikeni kwa ajili ya ngano na shayiri,
kwa sababu mavuno ya shambani yameharibiwa.
12 Mzabibu umekauka
na mtini umenyauka;
mkomamanga, mtende na mtofaa,
miti yote shambani, imekauka.
Hakika furaha yote ya mwanadamu
imeondoka.

*Wito wa kuomboleza*

13 Vaeni gunia, enyi makuhani, mwomboleze;
pigeni yowe, enyi mnaohudumu madhabahuni.
Njooni, vaeni gunia usiku kucha,

enyi mnaohudumu mbele za Mungu wangu;
kwa kuwa sadaka za nafaka na sadaka za kiny-
waji
zimezuiliwa kufika katika nyumba ya Mungu
wenu.
14 Tangazeni saumu takatifu;
liiteni kusanyiko takatifu.
Waiteni wazee
na wote wanaoishi katika nchi
waende katika nyumba ya Mwenyezi Mungu,
Mungu wenu,
wakamlilie Mwenyezi Mungu.

15 Ole kwa siku hiyo!
Kwa kuwa siku ya Mwenyezi Mungu iko
karibu;
itakuja kama uharibifu
kutoka kwa Mwenyezi.*

16 Je, chakula hakikukatiliwa mbali
mbele ya macho yetu:
furaha na shangwe
kutoka nyumba ya Mungu wetu?
17 Mbegu zinakauka
chini ya mabonge ya udongo.
Maghala yameachwa katika uharibifu,
maghala ya nafaka yamebomolewa,
kwa maana hakuna nafaka.
18 Jinsi gani ng'ombe wanavyolia!
Makundi ya mifugo yanahangaika
kwa sababu hawana malisho;
hata makundi ya kondoo yanateseka.

---

* **1:15** Mwenyezi hapa ina maana ya *Shaddai* kwa Kiebrania.

19 Kwako, Ee Mwenyezi Mungu, naita,
kwa kuwa moto umeteketeza
malisho ya mbugani
na miali ya moto imeunguza
miti yote shambani.
20 Hata wanyama pori wanakuonea shauku;
vijito vya maji vimekauka,
na moto umeteketeza
malisho yote ya mbugani.

# 2

*Jeshi la nzige*

1 Pigeni tarumbeta katika Sayuni;
pigeni mbiu katika mlima wangu mtakatifu.

Wote wanaoishi katika nchi na watetemeke,
kwa kuwa siku ya Mwenyezi Mungu inakuja.
Iko karibu,
2 siku ya giza na huzuni,
siku ya mawingu na utusitusi.
Kama mapambazuko yanavyosambaa
toka upande huu wa milima
hata upande mwingine,
jeshi kubwa na lenye nguvu linakuja.
Jambo kama hili halijakuwepo tangu zamani,
wala halitakuwepo tena kamwe
kwa vizazi vijavyo.

3 Mbele yao moto unateketeza,
nyuma yao miali ya moto
inawaka kwa nguvu.
Mbele yao nchi iko kama bustani ya Edeni,
nyuma yao ni jangwa lisilofaa:

hakuna kitu kinachowaepuka.
4 Wanaonekana kama farasi;
wanaenda mbio
kama askari wapanda farasi.
5 Wanatoa sauti kama magari ya vita,
wanaporukaruka juu ya vilele vya milima,
kama mlio wa miali ya moto ilayo mabua,
kama jeshi kubwa lililojipanga kwa ajili ya vita.

6 Wanapoonekana, mataifa yanakuwa katika maumivu makuu;
kila uso unabadilika rangi.
7 Wanashambulia kama mashujaa;
wanapanda kuta kama askari.
Wote wanatembea katika safu,
hawapotoshi safu zao.
8 Hakuna anayemsukuma mwenzake;
kila mmoja anaenda mbele moja kwa moja.
Wanapita katika vizuizi
bila kuharibu safu zao.
9 Wanaenda kasi kuingia mjini;
wanakimbia ukutani.
Wanaingia ndani ya nyumba;
kwa kuingilia madirishani kama wezi.

10 Mbele yao dunia inatikisika,
anga linatetemeka,
jua na mwezi vinatiwa giza,
na nyota hazitoi mwanga wake tena.
11 Mwenyezi Mungu anatoa mshindo wa ngurumo
mbele ya jeshi lake;
majeshi yake hayana idadi,

ni wenye nguvu nyingi
wale ambao hutii agizo lake.
Siku ya Mwenyezi Mungu ni kuu,
ni ya kutisha.
Ni nani anayeweza kuistahimili?

### *Rarueni mioyo yenu*

12 “Hata sasa,” asema Mwenyezi Mungu,
“nirudieni kwa mioyo yenu yote,
kwa kufunga, kwa kulia na kuomboleza.”

13 Rarueni mioyo yenu
na siyo mavazi yenu.
Mrudieni Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
kwa maana yeye ndiye mwenye neema
na mwingi wa huruma,
si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa upendo,
huona huruma, hujizuia kuleta maafa.
14 Ni nani ajuaye? Yeye aweza kugeuka na kuwa na huruma
na kuacha baraka nyuma yake:
sadaka za nafaka na sadaka za vinywaji
kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu.

15 Pigeni tarumbeta katika Sayuni,
tangazeni saumu takatifu,
liiteni kusanyiko takatifu.
16 Wakusanyeni watu,
wekeni wakfu kusanyiko;
waleteni pamoja wazee,
wakusanyeni watoto,
wale wanyonyao maziwa.
Bwana arusi na atoke chumbani mwake

na bibi arusi naye atoke katika chumba chake.
17 Makuhani, ambao wanahudumu mbele za Mwenyezi Mungu,
na walie katikati ya ukumbi
wa Hekalu na madhabahu.
Waseme, “Wahurumie watu wako, Ee Mwenyezi Mungu.
Usifanye urithi wako kitu cha kudharauliwa,
neno la dhihaka kati ya mataifa.
Kwa nini wasemezane miongoni mwao,
‘Yuko wapi Mungu wao?’ ”

### *Jibu la Mwenyezi Mungu*

18 Kisha Mwenyezi Mungu atakuwa na wivu kwa ajili ya nchi yake
na kuwa na huruma juu ya watu wake.
19 Mwenyezi Mungu atawajibu:
“Ninawapelekea nafaka,
mvinyo mpya na mafuta,
vya kuwatosha ninyi
hadi mridhike kabisa;
kamwe sitawafanya tena
kitu cha kudharauliwa na mataifa.

20 “Nitafukuza jeshi la kaskazini likae mbali nanyi,
nikilisukuma ndani ya jangwa,
askari wa safu za mbele wakienda
ndani ya bahari ya mashariki
na wale wa safu za nyuma
katika bahari ya magharibi.
Uvundo wake utapaa juu;
harufu yake itapanda juu.”

Hakika ametenda mambo makubwa.
21 Usiogope, ee nchi;
furahi na kushangilia.
Hakika Mwenyezi Mungu ametenda mambo makubwa.
22 Msiogope, enyi wanyama pori,
kwa kuwa mbuga za malisho yenu
zinarudia ubichi.
Miti nayo inazaa matunda,
mtini na mzabibu inatoa utajiri wake.
23 Furahini, enyi watu wa Sayuni,
shangilieni katika Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
kwa kuwa amewapa mvua za vuli
kwa kipimo cha haki.
Anawapelekea mvua nyingi,
mvua ya vuli na ya masika, kama mwanzoni.
24 Sakafu za kupuria zitajaa nafaka,
mapipa yatafurika mvinyo mpya na mafuta.

25 “Nitawalipa kwa ajili ya miaka ile iliyoliwa na nzige:
parare, madumadu na tunutu,
jeshi langu kubwa ambalo
nililituma kati yenu.
26 Mtakuwa na wingi wa vyakula hadi mshibe,
na mtalisifu jina la Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
ambaye amefanya maajabu kwa ajili yenu;
kamwe watu wangu hawataaibishwa tena.
27 Ndipo mtajua kuwa mimi niko katika Israeli,
kuwa mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
na kwamba hakuna mwingine;

kamwe watu wangu hawataaibika tena.

*Siku ya Mwenyezi Mungu*

28 “Hata itakuwa, baada ya hayo,
nitamimina Roho wangu Mtakatifu juu ya wote wenye mwili.
Wana wenu wa kiume na wa kike watatabiri,
wazee wenu wataota ndoto,
na vijana wenu wataona maono.
29 Hata juu ya watumishi wangu, wanaume kwa wanawake,
katika siku zile nitamimina Roho wangu Mtakatifu.
30 Nami nitaonesha maajabu katika mbingu
na duniani:
damu, moto na mawimbi ya moshi.
31 Jua litageuzwa kuwa giza
na mwezi kuwa mwekundu kama damu,
kabla ya kuja siku ya Mwenyezi Mungu
ile kuu na ya kutisha.
32 Na kila mtu atakayeliitia
jina la Mwenyezi Mungu ataokolewa.
Kwa maana juu ya Mlima Sayuni na katika Yerusalemu
kutakuwa na wokovu,
kama Mwenyezi Mungu alivyosema,
miongoni mwa walionusurika
ambao Mwenyezi Mungu awaita.

# 3

*Mataifa yahukumiwa*

1 “Katika siku hizo na wakati huo,
nitakaporejesha neema ya Yuda na Yerusalemu,

2 nitayakusanya mataifa yote na kuyaleta
katika Bonde la Yehoshafati*.
Hapo nitaingia kwenye hukumu dhidi yao
kuhusu urithi wangu, watu wangu Israeli,
kwa kuwa waliwatawanya watu wangu
miongoni mwa mataifa
na kuigawa nchi yangu.
3 Waliwapigia kura watu wangu
na kuwauza wavulana ili kupata makahaba;
waliwauza wasichana
ili wapate kunywa mvinyo.
4 "Sasa una nini dhidi yangu, ee Tiro na Sidoni,
nanyi nchi zote za Ufilisti? Je, mnanilipiza kwa
yale niliyoyafanya? Kama mnalipa, mimi nitalip-
iza juu ya vichwa vyenu kwa kasi na kwa haraka
yale mliyoyatenda.
5 Kwa kuwa mlichukua fedha na dhahabu
yangu pia mkabeba hazina zangu nzuri sana
mkapeleka kwenye mahekalu yenu.
6 Mliwauza watu wa Yuda na Yerusalemu kwa
Wayunani, ili mpate kuwapeleka mbali na nchi
yao.
7 "Tazama nitawaamsha kutoka zile sehemu
mlizowauza, nami nitawalipiza juu ya vichwa
vyenu kile mlichofanya.
8 Nitawauza wana wenu wa kiume na wa kike
kwa watu wa Yuda, nao watawauza kwa Waseba,
taifa lililo mbali." Mwenyezi Mungu amesema.
9 Tangazeni hili miongoni mwa mataifa:
Jiandaeni kwa vita!
Amsha mashujaa!

* **3:2** Yehoshafati maana yake *Mwenyezi Mungu huhukumu* pia 3:12; hivyo maana yake ni *Bonde la Hukumu ya Mwenyezi Mungu.*

Wapiganaji wote wasogee karibu na kushambulia.
10 Majembe yenu yafueni yawe panga,
na miundu yenu ya kukatia iwe mikuki.
Aliye dhaifu na aseme,
“Mimi nina nguvu!”
11 Njooni haraka, ninyi mataifa yote kutoka pande zote,
kusanyikeni huko.

Shusha mashujaa wako, Ee Mwenyezi Mungu!

12 “Mataifa na yaamshwe;
na yasonge mbele kuelekea Bonde la Yehoshafati,
kwa kuwa nitaketi mahali pale
kuhukumu mataifa yote yaliyo kila upande.
13 Tia mundu,
kwa kuwa mavuno yamekomaa.
Njooni, mkanyage zabibu,
kwa kuwa shinikizo la kukamulia zabibu limejaa
na mapipa yanafurika:
kwa kuwa uovu wao ni mkubwa!”

14 Umati mkubwa, umati mkubwa
katika bonde la uamuzi!
Kwa kuwa siku ya Mwenyezi Mungu ni karibu
katika bonde la uamuzi.
15 Jua na mwezi vitatiwa giza,
na nyota hazitatoa mwanga wake tena.
16 Mwenyezi Mungu atanguruma kutoka Sayuni
na mshindo wa ngurumo kutoka Yerusalemu;

dunia na mbingu vitatikisika.
Lakini Mwenyezi Mungu atakuwa kimbilio la watu wake,
ngome imara kwa ajili ya watu wa Israeli.

### *Baraka kwa watu wa Mwenyezi Mungu*

17 “Ndipo mtajua kuwa Mimi, Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
nakaa Sayuni, mlima wangu mtakatifu.
Yerusalemu utakuwa mtakatifu;
kamwe wageni hawatauvamia tena.

18 “Katika siku hiyo milima itadondosha divai mpya,
na vilima vitatiririka maziwa;
mabonde yote ya Yuda yatatiririka maji.
Chemchemi itatiririka kutoka nyumba ya Mwenyezi Mungu
na kunywesha Bonde la Shitimu†.
19 Lakini Misri itakuwa ukiwa,
Edomu itakuwa jangwa tupu,
kwa sababu ya jeuri waliofanya kwa watu wa Yuda,
ambao katika nchi yao
walimwaga damu isiyo na hatia.
20 Yuda itakaliwa na watu milele
na Yerusalemu itadumu vizazi vyote.
21 Hatia yao ya damu, ambayo sijasamehe,
nitasamehe.”

Mwenyezi Mungu anakaa Sayuni!

† **3:18** au *Bonde la Migunga.*

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d